

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
RUTHU 1	RUTH 1
1:1 Ikawa zamani za Waamuzi walipoamua, kulikuwa na njaa katika nchi. Akaondoka mtu mmoja wa Bethlehemu ya Yuda, akaenda kukaa katika nchi ya Moabu, yeye na mkewe na wanawe wawili. –	1:1 In the days when the judges ruled, there was a famine in the land, and a man from Bethlehem in Judah, together with his wife and two sons, went to live for a while in the country of Moab.
1:2 Na jina la mtu huyo alitwa Elimeleki, na jina la mkewe Naomi, na majina ya wanawe wawili Maloni na Kiloni, Waefrathi wa Bethlehemu ya Yuda. Wakafika nchi ya Moabu, wakakaa huko. –	1:2 The man’s name was Elimelech, his wife’s name Naomi, and the names of his two sons were Mahlon and Kilion. They were Ephrathites from Bethlehem, Judah. And they went to Moab and lived there.
1:3 Akafa Elimeleki, mumewe Naomi; na yule mwanamke akasalia na wanawe wawili.	1:3 Now Elimelech, Naomi’s husband, died, and she was left with her two sons.
1:4 Nao wakaoa wake katika wanawake wa Moabu; na jina la mmoja alitwa Orpa, na jina la wa pili Ruthu. Wakakaa huko yapata miaka kumi.	1:4 They married Moabite women, one named Orpah and the other Ruth. After they had lived there about ten years,
1:5 Wakafa na Maloni na Kiloni wote wawili; na huyo mwanamke akawa amefiwa na wanawe wawili, na mumewe pia.	1:5 both Mahlon and Kilion also died, and Naomi was left without her two sons and her husband.
1:6 Ndipo alipoondoka, yeye na wakweze, ili kurudi kutoka nchi ya Moabu; maana huko katika nchi ya Moabu amesikia ya kwamba Bwana amewajilia watu wake na kuwapa chakula. –	1:6 When she heard in Moab that the Lord had come to the aid of his people by providing food for them, Naomi and her daughters-in-law prepared to return home from there.
1:7 Basi akatoka pale alipokuwapo, na wakweze wawili pamoja naye; wakashika njia ili kurudi mpaka nchi ya Yuda.	1:7 With her two daughters-in-law she left the place where she had been living and set out on the road that would take them back to the land of Judah.
1:8 Kisha Naomi akawaambia wakweze wawili, Nendeni sasa mkarejee kila mmoja nyumbani kwa mamaye; Bwana na awatendee mema ninyi, kama ninyi mlivyowatendea mema hao waliofariki na mimi pia. –	1:8 Then Naomi said to her two daughters-in-law, “Go back, each of you, to your mother’s home. May the Lord show kindness to you, as you have shown to your dead and to me.
1:9 Bwana na awajalie kuona raha kila mmoja nyumbani kwa mumewe. Kisha akawabusu; nao wakapaza sauti zao wakalia. –	1:9 May the Lord grant that each of you will find rest in the home of another husband.” Then she kissed them and they wept aloud.
1:10 Wakamwambia, La, sivyo; lakini tutarudi pamoja nawe kwa watu wako.	1:10 and said to her, “We will go back with you to your people.”
1:11 Naye Naomi akasema, Enyi wanangu, mrejee; kwani kufuatana na mimi? Je! Mimi ninao watoto wa kume tena tumboni mwangu, hata wawe waume zenu? –	1:11 But Naomi said, “Return home, my daughters. Why would you come with me? Am I going to have any more sons, who could become your husbands?
1:12 Enyi wanangu, mrejee; nendeni zenu; kwa kuwa mimi ni mzee, siwezi kupata mume tena. Kama ningesema, Natumaini; kama ningepata mume hata usiku huu, na kuzaa watoto wa kume;	1:12 Return home, my daughters; I am too old to have another husband. Even if I thought there was still hope for me—even if I had a husband tonight and then gave birth to sons—

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
1:13 je! Mngesubiri hata watakapokuwa watu wazima? Mngejizua msiwe na waume? La, sivyo, wanangu; maana ni vigumu kwangu kuliko kwenu, kwa sababu mkono wa Bwana umetoka juu yangu. –	1:13 would you wait until they grew up? Would you remain unmarried for them? No, my daughters. It is more bitter for me than for you, because the Lord's hand has gone out against me!"
1:14 Nao wakapaza sauti zao, wakalia tena, na Orpa akambusu mkwewe, lakini Ruthu akaambatana naye. –	1:14 At this they wept again. Then Orpah kissed her mother-in-law good-by, but Ruth clung to her.
1:15 Naye akasema, Tazama, shemeji yako amerejea kwa watu wake, na kwa mungu wake; basi ur ejee wewe umfuate shemeji yako. –	1:15 "Look," said Naomi, "your sister-in-law is going back to her people and her gods. Go back with her."
1:16 Naye Ruthu akasema, Usinisihi nikuache, Nirejee nisifuatane nawe; Maana wewe uendako nitakwenda, Na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu;	1:16 But Ruth replied, "Don't urge me to leave you or to turn back from you. Where you go I will go, and where you stay I will stay. Your people will be my people and your God my God.
1:17 Pale utakapokufa nitakufa nami, Na papo hapo nitazikwa; Bwana anitende vivyo na kuzidi, Ila kufa tu kutatutenga wewe nami.	1:17 Where you die I will die, and there I will be buried. May the Lord deal with me, be it ever so severely, if anything but death separates you and me."
1:18 Basi alipomwona kuwa amekaza nia yake kufuatana naye, aliacha kusema naye. -	1:18 When Naomi realized that Ruth was determined to go with her, she stopped urging her.
1:19 Hivyo hao wakaendelea wote wawili hata walipofika Bethlehemu. Na ikawa walipofika Bethlehemu, mji wote ulitaharuki kwa habari zao. Nao wanawake wakasema, Je! Huyu ni Naomi? –	1:19 So the two women went on until they came to Bethlehem. When they arrived in Bethlehem, the whole town was stirred because of them, and the women exclaimed, "Can this be Naomi?"
1:20 Akawaambia, Msiniite Naomi a, niiteni Mara b, kwa sababu Mwenyezi Mungu amenitenda mambo machungu sana.	1:20 "Don't call me Naomi," she told them. "Call me Mara, because the Almighty has made my life very bitter.
1:21 Mimi nalitoka hali nimejaa, naye Bwana amenirudisha sina kitu, kwani kuniita Naomi, ikiwa Bwana ameshuhudia juu yangu, na Mwenyezi Mungu amenitesa? –	1:21 I went away full, but the Lord has brought me back empty. Why call me Naomi? The Lord has afflicted me; the Almighty has brought misfortune upon me."
1:22 Basi Naomi akarudi; pamoja na Ruthu Mmoabi, mkwewe; ambao walirudi kutoka nchi ya Moabu; nao wakafika Bethlehemu mwanzo wa mavuno ya shayiri. -	1:22 So Naomi returned from Moab accompanied by Ruth the Moabitess, her daughter-in-law, arriving in Bethlehem as the barley harvest was beginning.
RUTHU 2	RUTH 2
2:1 Basi huyo Naomi alikuwa na ndugu ya mumewe, mtu mkuu mwenye mali, wa jamaa yake Elimeleki, na jina lake aliitwa Boazi. –	2:1 Now Naomi had a relative on her husband's side, from the clan of Elimelech, a man of standing, whose name was Boaz.

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
2:2 Naye Ruthu Mmoabi akamwambia Naomi, Sasa niende kondeni, niokote masazo ya masuke nyuma yake yule ambaye nitaona kibali machoni pake. Akamwambia, Haya, mwanangu, nenda. –	2:2 And Ruth the Moabitess said to Naomi, “Let me go to the fields and pick up the leftover grain behind anyone in whose eyes I find favor.” Naomi said to her, “Go ahead, my daughter.”
2:3 Basi akaenda, akaja akaokota masazo kondeni nyuma ya wavunaji; na bahati yake ikamtukia kwamba akaifika sehemu ya shamba iliyokuwa mali yake huyo Boazi, ambaye alikuwa wa jamaa yake Elimeleki.	2:3 So she went out and began to glean in the fields behind the harvesters. As it turned out, she found herself working in a field belonging to Boaz, who was from the clan of Elimelech.
2:4 Na tazama, Boazi akaja kutoka Bethlehemu kawaamkia wavunaji, akasema, Bwana akae nanyi. Nao wakamwitikia, Bwana na akubariki. –	2:4 Just then Boaz arrived from Bethlehem and greeted the harvesters, “The Lord be with you!” “The Lord bless you!” they called back.
2:5 Kisha Boazi akamwuliza mtumishi aliyewasimamia wavunaji, Na huyu je! Ni msichana wa nani?	2:5 Boaz asked the foreman of his harvesters, “Whose young woman is that?”
2:6 Yule msimamizi aliyewasimamia wavunaji akajibu, akasema, Ni yule msichana Mmoabi aliyerudi pamoja na Naomi, kutoka nchi ya Moabu; -	2:6 The foreman replied, “She is the Moabitess who came back from Moab with Naomi.
2:7 naye akasema, Tafadhali niruhusu kuokota masazo, na kukusanya nyuma ya wavunaji kati ya miganda; basi akaja, naye ameshinda tangu asubuhi hata sasa, isipokuwa alikaa nyumbani kitambo kidogo.	2:7 She said, ‘Please let me glean and gather among the sheaves behind the harvesters.’ She went into the field and has worked steadily from morning till now, except for a short rest in the shelter.”
2:8 Basi Boazi akamwambia Ruthu, Mwanangu, sikiliza; wewe usiende kuokota masazo katika shamba lingine, wala usiondoke hapa, lakini ukae papa hapa karibu na wasichana wangu.	2:8 So Boaz said to Ruth, “My daughter, listen to me. Don’t go and glean in another field and don’t go away from here. Stay here with my servant girls.
2:9 Macho yako na yaelekee konde walivunalo, ufuatane nao; je! Sikuwaagiza vijana wasikuguse? Tena, ukiona kiu, uende kwenye vyombo, nawe uyanaye waliyoyateka hao vijana.	2:9 Watch the field where the men are harvesting, and follow along after the girls. I have told the men not to touch you. And whenever you are thirsty, go and get a drink from the water jars the men have filled.”
2:10 Ndipo aliposujudia, akainama mpaka nchi, akamwambia, Jinsi gani nimepata kibali machoni pako, hata ukanifahamu, mimi niliye mgeni? –	2:10 At this, she bowed down with her face to the ground. She exclaimed, “Why have I found such favor in your eyes that you notice me—a foreigner?”
2:11 Naye Boazi akajibu, akamwambia, Nimeelezwa sana yote uliyomfanyia mkweo, tangu alipokufa mumeo; na jinsi ulivyowaacha baba yako na mama yako, na nchi yako uliyozaliwa, ukawafikilia watu usiowajua tangu hapo. –	2:11 Boaz replied, “I’ve been told all about what you have done for your mother-in-law since the death of your husband—how you left your father and mother and your homeland and came to live with a people you did not know before.

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
2:12 Bwana akujazi kwa kazi yako, nawe upewe thawabu kamili na Bwana, Mungu wa Israeli, ambaye umekuja kukimbilia chini ya mabawa yake. –	2:12 May the Lord repay you for what you have done. May you be richly rewarded by the Lord, the God of Israel, under whose wings you have come to take refuge.”
2:13 Ndipo aliposema, Bwana wangu, na nipate kibali machoni pako; kwa sababu wewe umeniburudisha moyo, na kumwambia mema mjakazi wako, ingawa mimi si kama mmojawapo wa wajakazi wako. -	2:13 “May I continue to find favor in your eyes, my lord,” she said. “You have given me comfort and have spoken kindly to your servant—though I do not have the standing of one of your servant girls.”
2:14 Tena wakati wa chakula huyo Boazi akamwambia, Karibu kwetu, ule katika mkate wetu, na ulichovye tonge lako katika siki yetu. Basi akaketi pamoja na wavunaji, nao wakampitishia bisi, naye akala akashiba, hata akasaza.	2:14 At mealtime Boaz said to her, “Come over here. Have some bread and dip it in the wine vinegar.” When she sat down with the harvesters, he offered her some roasted grain. She ate all she wanted and had some left over.
2:15 Naye alipoinuka tena ili aende kuokota masazo, huyo Boazi aliwaagiza vijana wake akisema, Mwacheni aokote hata kati ya miganda, wala msimkeme.	2:15 As she got up to glean, Boaz gave orders to his men, “Even if she gathers among the sheaves, don’t embarrass her.
2:16 Tena mtoleeni kidogo katika matita na kukiacha, na akiokote, wala msimkataze.	2:16 Rather, pull out some stalks for her from the bundles and leave them for her to pick up, and don’t rebuke her.”
2:17 Basi Ruthu akaokota masazo kondeni hata jioni; kisha akazipura zile nafaka alizoziokota, zikawa yapata efa moja ya shayiri.	2:17 So Ruth gleaned in the field until evening. Then she threshed the barley she had gathered, and it amounted to about an ephah.
2:18 Akajitwika, akaenda zake mjini. Akamwonyesha mkwewe zile alizoziokota; akavitoe vile vyakula alivyovisaza alipokwisha kushiba, akampa.	2:18 She carried it back to town, and her mother-in-law saw how much she had gathered. Ruth also brought out and gave her what she had left over after she had eaten enough.
2:19 Basi mkwewe akamwuliza, Je! Umeokota wapi leo? Umefanya kazi wapi? Na abarikiwe yeye aliyekufahamu. Naye akamwarifu mkwewe ni nani ambaye alifanya kazi kwake, akasema, Yule mtu niliyefanya kazi kwake leo jina lake aitwa Boazi.	2:19 Her mother-in-law asked her, “Where did you glean today? Where did you work? Blessed be the man who took notice of you!” Then Ruth told her mother-in-law about the one at whose place she had been working. “The name of the man I worked with today is Boaz,” she said.
2:20 Naye Naomi akamwambia mkwewe, Na abarikiwe huyo na Bwana, ambaye hakuuacha wema wake, wala kwa hao walio hai wala kwao waliokufa. Kisha Naomi akamwambia, Mtu huyu ni wa mbari yetu, mmojawapo wa jamaa yetu aliye karibu. –	2:20 “The Lord bless him!” Naomi said to her daughter-in-law. “He has not stopped showing his kindness to the living and the dead.” She added, “That man is our close relative; he is one of our kinsman-redeemers.”
2:21 Naye Ruthu Mmoabi akasema, Naam, akaniambia, Ukae papa hapa karibu na vijana wangu, hata watakapomaliza mavuno yangu yote.	2:21 Then Ruth the Moabitess said, “He even said to me, ‘Stay with my workers until they finish harvesting all my grain.’”

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
2:22 Kisha Naomi akamwambia Ruthu mkwewe, Mwanangu, ni vizuri wewe ufuatane na wasichana wake, wala watu wasikukute katika konde linginelo lote.	2:22 Naomi said to Ruth her daughter-in-law, “It will be good for you, my daughter, to go with his girls, because in someone else’s field you might be harmed.”
2:23 Hivyo yeye akafuatana na wasichana wake Boazi na kuokota, hata mwisho wa mavuno ya shayiri na mavuno ya ngano pia; naye alikuwa akikaa kwa mkwewe.	2:23 So Ruth stayed close to the servant girls of Boaz to glean until the barley and wheat harvests were finished. And she lived with her mother-in-law.
RUTHU 3	RUTH 3
3:1 Kisha Naomi akamwambia mkwewe, Je! Mwanangu, si vizuri nikutafutie raha, ili upate mema? –	3:1 One day Naomi her mother-in-law said to her, “My daughter, should I not try to find a home for you, where you will be well provided for?”
3:2 Basi na huyu Boazi, je! Siye wa mbari yetu, ambaye ulikuwapo pamoja na wasichana wake? Tazama, usiku wa leo atakuwa akipepeta shayiri pale ugani. –	3:2 Is not Boaz, with whose servant girls you have been, a kinsman of ours? Tonight he will be winnowing barley on the threshing floor.
3:3 Basi wewe oga, ujjipake mafuta ujivike mavazi yako, kisha uende kwenye uga; walakini usijionyeshe kwake mtu yule, ila atakapokwisha kula na kunywa. –	3:3 Wash and perfume yourself, and put on your best clothes. Then go down to the threshing floor, but don’t let him know you are there until he has finished eating and drinking.
3:4 Nayoy itakuwa wakati atakapolala, utapaangalia mahali alalapo, nawe uingie, uifunue miguu yake ujilaze hapo; na yeye atakuambia utakalofanya.	3:4 When he lies down, note the place where he is lying. Then go and uncover his feet and lie down. He will tell you what to do.”
3:5 Akamwambia, Hayo yote unenayo mimi nitayafanya. -	3:5 “I will do whatever you say,” Ruth answered.
3:6 Basi akashuka mpaka ugani; akafanya yote kama vile mkwewe alivyomwagiza.	3:6 So she went down to the threshing floor and did everything her mother-in-law told her to do.
3:7 Ikawa huyo Boazi alipokwisha kula na kunywa, na moyo wake umekunjuka, alikwenda kulala penye mwisho wa chungu ya nafaka; na huyo mwanamke akaja taratibu, akaifunua miguu yake, akajilaza papo hapo. –	3:7 When Boaz had finished eating and drinking and was in good spirits, he went over to lie down at the far end of the grain pile. Ruth approached quietly, uncovered his feet and lay down.
3:8 Na ikawa usiku wa manane yule mtu akasituka, akajigeuza; na kumbe! Yupo mwanamke amelala miguuni pake.	3:8 In the middle of the night something startled the man, and he turned and discovered a woman lying at his feet.
3:9 Akasema, Ama! Ni nani wewe? Akamjibu, Ni mimi, Ruthu, mjakazi wako; uitande nguo yako juu ya mjakazi wako; kwa kuwa ndiwe wa jamaa aliye karibu. –	3:9 “Who are you?” he asked. “I am your servant Ruth,” she said. “Spread the corner of your garment over me, since you are a kinsman-redeemer.”
3:10 Akamwambia, Mwanangu, ubarikiwe na Bwana; umezidi kuonyesha fadhili zako mwisho kuliko mwanzo, kwa vile usivyowafuata vijana, kama ni maskini kama ni matajiri. –	3:10 “The Lord bless you, my daughter,” he replied. “This kindness is greater than that which you showed earlier: You have not run after the younger men, whether rich or poor.

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
3:11 Basi, mwanangu, usiogope; mimi nitakufanyia yote uyanenayo; kwa maana mji wote pia wa watu wangu wanakujua ya kwamba u mwanamke mwema. –	3:11 And now, my daughter, don't be afraid. I will do for you all you ask. All my fellow townsmen know that you are a woman of noble character.
3:12 Tena ndiyo kweli ya kuwa mimi ni wa jamaa yako aliye karibu; lakini kuna mtu wa jamaa aliye karibu kuliko mimi. –	3:12 Although it is true that I am near of kin, there is a kinsman-redeemer nearer than I.
3:13 Wewe ungoje usiku huu; kisha, asubuhi, kama akikubali kukufanyia impasavyo jamaa, haya, na akufanyie; lakini ikiwa hataki yeye, basi mimi nitakufanyia impasavyo jamaa; Bwana aishivyo. Ulale wewe hata asubuhi. –	3:13 Stay here for the night, and in the morning if he wants to redeem, good; let him redeem. But if he is not willing, as surely as the Lord lives I will do it. Lie here until morning.”
3:14 Hivyo huyo mwanamke akalala miguuni pake hata asubuhi; akaondoka mapema asijaweza mtu kumtambua mwenziwe; maana Boazi amesema, Isijulikane kabisa ya kuwa mwanamke alifika penye uga. –	3:14 So she lay at his feet until morning, but got up before anyone could be recognized; and he said, “Don't let it be known that a woman came to the threshing floor.”
3:15 Tena alisema, Lete hapa shela yako uliyoivaa, uishike; naye akaishika; naye akampimia vipimo sita vya shayiri akamtwika; kisha huyo mwanamke akaenda zake mjini.	3:15 He also said, “Bring me the shawl you are wearing and hold it out.” When she did so, he poured into it six measures of barley and put it on her. Then he went back to town.
3:16 Basi alipofika kwa mkwewe, huyo akamwuliza, Je! Mwanangu, imekuwaje? Akamwambia yote yule mtu aliyomfanyia.	3:16 When Ruth came to her mother-in-law, Naomi asked, “How did it go, my daughter?” Then she told her everything Boaz had done for her
3:17 Akasema, Na vipimo hivi sita vya shayiri amenipa; maana akaniambia, Usiende kwa mkweo mikono mitupu.	3:17 and added, “He gave me these six measures of barley, saying, ‘Don't go back to your mother-in-law empty-handed.’”
3:18 Naye mkwewe akasema, Basi, mwanangu, tulia; hata utakapojua jinsi litakavyotukia jambo hili; kwa sababu mtu huyu hataridhika, asipolimaliza jambo hilo leo.	3:18 Then Naomi said, “Wait, my daughter, until you find out what happens. For the man will not rest until the matter is settled today.”
RUTHU 4	RUTH 4
4:1 Basi Boazi akakwea kwenda mpaka langoni, akaketi pale; na tazama, yule mtu wa jamaa aliyekuwa karibu, ambaye Boazi amemnena, akapita. Naye akamwita, Haya! Wewe, karibu, uketi hapa. Naye akaja akaketi. –	4:1 Meanwhile Boaz went up to the town gate and sat there. When the kinsman-redeemer he had mentioned came along, Boaz said, “Come over here, my friend, and sit down.” So he went over and sat down.
4:2 Kisha akatwaa watu kumi miongoni mwa wazee wa mji, akawaambia, Ninyi nanyi, ketini hapa. Wakaketi. –	4:2 Boaz took ten of the elders of the town and said, “Sit here,” and they did so.
4:3 Kisha akamwambia yule jamaa, Huyu Naomi, aliyerudi hapa kutoka nchi ya Moabu, anauza sehemu ya ardhi aliyokuwa nayo ndugu yetu, Elimeleki;	4:3 Then he said to the kinsman-redeemer, “Naomi, who has come back from Moab, is selling the piece of land that belonged to our brother Elimelech.

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
<p>4:4 nami ilikuwa nia yangu nikujulishe wewe, na kukuambia, Uinunue mbele ya hawa waliopo na mbele ya wazee wa watu wangu. Kama wewe utaikomboa, haya, uikomboe; lakini kama hutaikomboa, uniambie ili nijue mimi; kwa kuwa hakuna mtu wa kuikomboa ila wewe, na baada yako ni mimi. Naye akasema, Nitaikomboa mimi. –</p>	<p>4:4 I thought I should bring the matter to your attention and suggest that you buy it in the presence of these seated here and in the presence of the elders of my people. If you will redeem it, do so. But if you will not, tell me, so I will know. For no one has the right to do it except you, and I am next in line.” “I will redeem it,” he said.</p>
<p>4:5 Ndipo Boazi aliposema, Siku ile utakapolinunua shamba mkononi mwa Naomi, unamnunua Ruthu pia, huyu Mmoabi, mkewe marehemu, ili makusudi umwinulie marehemu jina katika urithi wake. –</p>	<p>4:5 Then Boaz said, “On the day you buy the land from Naomi and from Ruth the Moabitess, you acquire the dead man’s widow, in order to maintain the name of the dead with his property.”</p>
<p>4:6 Basi yule jamaa aliyekuwa wa karibu akasema, Mimi sitaweza kulikomboa kwa nafsi yangu, nisije nikauharibu urithi wangu mwenyewe; basi haki yangu ya kulikomboa ujichukulie wewe, maana mimi sitaweza kulikomboa. –</p>	<p>4:6 At this, the kinsman-redeemer said, “Then I cannot redeem it because I might endanger my own estate. You redeem it yourself. I cannot do it.”</p>
<p>4:7 Basi hii ilikuwa desturi zamani za kale katika Israeli, kwa habari ya kukomboa na kubadiliana, ili kuyahakikisha yote; mtu huvua kiatu chake na kumpa mwenziwe; ndivyo walivyohakikisha neno katika Israeli. –</p>	<p>4:7 (Now in earlier times in Israel, for the redemption and transfer of property to become final, one party took off his sandal and gave it to the other. This was the method of legalizing transactions in Israel.)</p>
<p>4:8 Basi yule jamaa akamwambia Boazi, Wewe ujinunulie mwenyewe. Akavua kiatu chake.</p>	<p>4:8 So the kinsman-redeemer said to Boaz, “Buy it yourself.” And he removed his sandal.</p>
<p>4:9 Naye Boazi akawaambia wale wazee na watu wote, Leo hivi ninyi ni mashahidi ya kwamba mimi nimenunua yote yaliyokuwa ya Elimeleki, na yote yaliyokuwa ya Kilioni na Maloni, mkononi mwa Naomi.</p>	<p>4:9 Then Boaz announced to the elders and all the people, “Today you are witnesses that I have bought from Naomi all the property of Elimelech, Kilion and Mahlon.</p>
<p>4:10 Tena, huyu Ruthu Mmoabi, mkewe Maloni, nimemnunua awe mke wangu, makusudi nipate kumwinulia marehemu jina katika urithi wake, jina lake marehemu lisikatike miongoni mwa ndugu zake, wala langoni pa mji wake; leo hivi ninyi ni mashahidi. –</p>	<p>4:10 I have also acquired Ruth the Moabitess, Mahlon’s widow, as my wife, in order to maintain the name of the dead with his property, so that his name will not disappear from among his family or from the town records. Today you are witnesses!”</p>
<p>4:11 Na watu wote waliokuwapo langoni, na wale wazee, wakasema, Naam, sisi ni mashahidi. Bwana na amfanye mwanamke huyu aingiaye nyumbani mwako kuwa kama Raheli na kama Lea, wale wawili walioijenga nyumba ya Israeli. Nawe ufanikiwe katika Efrata, na kuwa mashuhuri katika Bethlehemu. –</p>	<p>4:11 Then the elders and all those at the gate said, “We are witnesses. May the Lord make the woman who is coming into your home like Rachel and Leah, who together built up the house of Israel. May you have standing in Ephrathah and be famous in Bethlehem.</p>

SWAHILI	NEW INTERNATIONAL VERSION
4:12 Nyumba yako na ifanane na nyumba yake Peresi, ambaye kwamba Tamari alimzalia Yuda, kwa wazao atakaokupa Bwana katika mwanamke huyu. -	4:12 Through the offspring the Lord gives you by this young woman, may your family be like that of Perez, whom Tamar bore to Judah.”
4:13 Basi Boazi akamtwaa Ruthu, naye akawa mke wake; naye akaingia kwake, na Bwana akamjalia kuchukua mimba, naye akazaa mtoto wa kiume. –	4:13 So Boaz took Ruth and she became his wife. Then he went to her, and the Lord enabled her to conceive, and she gave birth to a son.
4:14 Nao wale wanawake wakamwambia Naomi, Na ahimidiwe Bwana, asiyekuacha leo hali huna wa jamaa aliye karibu; jina lake huyu na liwe kuu katika Israeli. –	4:14 The women said to Naomi: “Praise be to the Lord, who this day has not left you without a kinsman-redeemer. May he become famous throughout Israel!
4:15 Naye atakurejezea uhai wako, na kukuangalia katika uzee wako; kwa maana mkweo, ambaye akupenda, naye anakufaa kuliko watoto saba, ndiye aliyemzaa. -	4:15 He will renew your life and sustain you in your old age. For your daughter-in-law, who loves you and who is better to you than seven sons, has given him birth.”
4:16 Basi Naomi akamtwaa yule mtoto, akamweka kifuani pake, akawa mlezi wake.	4:16 Then Naomi took the child, laid him in her lap and cared for him.
4:17 Nao wale wanawake waliokuwa jirani zake wakampa jina, wakisema, Naomi amezaliwa mwana; wakamwita jina lake Obedi; yeye ndiye baba yake Yese, aliye baba yake Daudi. -	4:17 The women living there said, “Naomi has a son.” And they named him Obed. He was the father of Jesse, the father of David.
4:18 Hivi ndivyo vizazi vya Peresi; Peresi alimzaa Hesroni; -	4:18 This, then, is the family line of Perez: Perez was the father of Hezron,
4:19 na Hesroni akamzaa Ramu; na Ramu akamzaa Aminadabu;	4:19 Hezron the father of Ram, Ram the father of Amminadab,
4:20 na Aminadabu akamzaa Nashoni; na Nashoni akamzaa Salmoni; -	4:20 Amminadab the father of Nahshon, Nahshon the father of Salmon,
4:21 na Salmoni akamzaa Boazi; na Boazi akamzaa Obedi;	4:21 Salmon the father of Boaz, Boaz the father of Obed,
4:22 na Obedi akamzaa Yese; na Yese akamzaa Daudi.	4:22 Obed the father of Jesse, and Jesse the father of David.